# KUMBUKUMBU ZA SHUGHULI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI

KINONDONI MUNICIPAL COUNCIL

## MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KILICHOFANYIKA TAREHE 25/10/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA MANISPAA ULIOPO MAGOMENI.

## WAJUMBE WALIOHUDHURIA:

| NA. | JINA | CHEO/WADHIFA |
| --- | --- | --- |
| 1. | Mh. Songoro Mnyonge | Mwenyekiti/Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni |
| 2. | Mh. Kheri Missinga | Naibu Meya na Diwani wa Kata ya Bunju |
| 3. | Mh. Noordin Y. Hassan | Diwani wa Kata ya Magomeni. |
| 4. | Mh. Anna Lukindo | Diwani wa Kata ya Mbezi Juu |
| 5. | Mh. Manfred C. Lyoto | Diwani wa Kata ya Mzimuni |
| 6. | Mh. Leonard T. Manyama | Diwani wa Kata ya Wazo |
| 7. | Mh. Abdallah Aziz | Diwani wa Kata ya Tandale |
| 8. | Mh. Luca H. Neghest | Diwani wa Kata ya Msasani |

## KATIBU:

1. Shedrack R. Maximillian - Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa.

## WAJUMBE WASIOHUDHURIA:

Mh. Josephat Gwajima – Kwa Taarifa

Mh. Janeth Mahawanga – Kwa Taarifa

Mh. Tarimba Abbas - Kwa Taarifa

Mh. Janeth Mahawanga - Kwa Taarifa

Mh. Michael . J. Urio - Kwa Taarifa.

## SEKRETARIETI .

1. Deodatus Mapunda – Katibu Wa Kamati wa Manispaa.
2. Jacob Mbaga – Katibu Wa Kamati
3. Josephine Sanga – Katibu Wa Kamati

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA:**

| NA. | JINA | CHEO/WADHIFA |
|---|---|---|
| 1. | Onesmo R. Mwonga | Mweka Hazina wa Manispaa. |
| 2. | Fauzia Nombo | Afisa Utumishi Mkuu Manispaa |
| 3. | Eric Kilangwa | Mchumi wa Manispaa |
| 4. | Dr. Samwel Laizer | Mganga Mkuu wa Manispaa |
| 5. | Salumu Yusuph | Afisa Tehama wa Manispaa |
| 6. | Dr. Patricia Henjewele | Afisa Mifugo wa Manispaa |
| 7. | Geofrey Mwamsojo | Kaimu Afisa Mipangomiji wa Manispaa |
| 8. | Davis Sabas | Mkaguzi wa Ndani wa Manispaa |
| 9. | Elinaike Kombe | Kny. Katibu TSC |
| 10. | Hussein Ugulum | Mwanasheria wa Manispaa |
| 11. | Salum Ramadhani | Kny. Afisa Elimu Msingi wa Manispaa |
| 12. | Salum Chitale | Afisa Tarafa Kawe |
| 13. | Rahma Kondo | Afisa Tarafa Kinondoni |
| 14. | Stella Msofe | DAS - Kinondoni |
| 15. | John Deogratius | Kny. Afisa Maendeleo ya Jamii wa Manispaa. |
| 16. | Hilda H. Temu | Kny. Afisa Kilimo |
| 17. | Vumilia Tigwela | Afisa Ugavi wa Manispaa |
| 18. | Mkelewe Tungaraza | Kaimu Mhandisi wa Manispaa |
| 19. | Selemani Kitururu | Kaimu Afisa Usafishaji wa Manispaa |
| 20. | Mtundi Nyamhanga | Afisa Elimu Sekondari wa Manispaa |
| 21. | Sebastian Mhowera | Afisa Habari |
| 22. | Magreth J. Mangasa | Afisa Maendeleo ya Jamii |

**Agenda za Kikao cha tarehe 25/10/2021.**

i. Kufungua Kikao.

ii. Kupitia na kuidhinisha agenda za Kikao.

iii. (a) Matumizi ya fedha kiasi cha **Tshs 3,348,225,807.18** zilizopokelewa nje ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

(b). Maombi ya mabadiliko ya kazi za maeneo ya ujenzi wa shule za sekondari kulingana na hali halisi ya maeneo ya shule zetu.

(c) Taarifa ya nyongeza ya mpango wa manunuzi kwa mwaka 2021/2022.

iv. Kujadili Taarifa ya Utoaji wa Mikopo Kwa Vikundi Katika Manispaa ya Kinondoni.

v. Kufunga Kikao.

**1/FM/21 Kufungua Kikao.**

Katibu wa Kamati aliwakaribisha Wajumbe wote waliohudhuria kwenye Kikao hiki. Alieleza kuwa Kikao hiki ni maalum kwa ajili ya kujadili mapokezi ya fedha za Uviko -19 ambazo zimetolewa na Mh. Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania. Baada ya hapo alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue Kikao.

Mwenyekiti aliwakaribisha na kueleza kuwa Kikao hiki ni maalum kama alivyoeleza Katibu. Aliwaomba Wajumbe watoe hoja zao kwa ajili ya kufanikisha Kikao hiki. Baada ya hapo, alifungua Kikao saa 6.10 mchana.

**2/FM/21 Kupitia na Kuidhinisha agenda za Kikao.**

Wajumbe walipitia agenda zilizowasilishwa na kukubaliana kuwa zijadiliwe kama zilivyowasilishwa.

**3/FM/21 (a) Matumizi ya Fedha Kiasi cha Shilingi 3,348,225,807.18 Zilizopokelewa Nje ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022.**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni inaendelea na utekelezaji wa Mpango na Bajeti wa Mwaka 2021/22. Aidha, Halmashauri yetu imepokea fedha kiasi cha Shilingi **3,348,225,807.18** kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuendesha kampeni ya chanjo ya UVIKO 19 **(72,808,667.60)**, Ujenzi wa miundombinu ya elimu Msingi kupitia EP4R **(55,417,139.58)**, Ujenzi wa madarasa **146** katika Shule za Sekondari **(2,920,000,000.00)** na ujenzi wa Jengo la huduma ya dharura **(300,000,000.00)** kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19 ambazo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

**Jedwali Na.1 Mchangano wa fedha kwa vyanzo.**

| NA | CHANZO CHA FEDHA | SHUGHULI | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1. | Chanjo ya UVIKO 19 | Kampeni ya Chanjo ya UVIKO 19 | 72,808,667.60 |
| 2. | EP4R | Ujenzi wa miundombinu ya elimu Msingi (Vyoo na visima | 55,417,139.58 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | vya maji) | |
| 3. | Mpango wa UVIKO-19 | Ujenzi wa Jengo la huduma ya dharura | 300,000,000.00 |
| 4. | Mpango wa UVIKO-19 | Ujenzi wa madarasa 146 katika Shule za Sekondari | 2,920,000,000.00 |
| | **JUMLA** | | **3,348,225,807.18** |

Kwa kuwa fedha hizi hazikuwepo kwenye Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2021/2022 ambao Baraza la Madiwani lilipitisha Januari Mwaka 2021, hivyo maombi haya yanawasilishwa ili kuomba idhini ya kuendelea na utekelezaji wa shughuli husika.

Pamoja na taarifa hii mchanganuo wa miradi husika kwa fedha hizi kwa kila chanzo umeambatanishwa.

**Hoja mbalimbali za Wajumbe.**

- Kata za Kinondoni na Tandale hazijawahi kuwa na Sekondari, aidha hata fedha zikiletwa Kata hizo haziangaliwi.
- Kata ya Magomeni. Jitihada zifanyike kuongeza idadi ya madarasa yaliyopungua.

**Azimio.**

Wajumbe walipitisha matumizi ya fedha kiasi cha shilingi 3,348,225,807.18 zilizopokelewa Nje ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Aidha walitoa idhini ya kuendelea na utekelezaji wa shughuli husika kama ilivyowasilishwa. Tazama Kiambatanisho.

**Pongezi.**

Wajumbe walitoa pongezi kwa Mh. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuleta fedha hizi katika Manispaa ya Kinondoni.

(b) **Maombi ya Mabadiliko ya Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa kwa fedha za Uviko – 19.**

1. **Utangulizi.**

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni imepokea kiasi cha Tsh. **2,920,000,000.00** fedha **za Uviko-19** kwa ajili ya ujenzi wa madarasa **146** kwa shule za sekondari Fedha hizo zimeelekezwa kwa shule zetu zote **29** ambazo

zimesajiliwa ili kuwezesha kupunguza changamoto za Madarasa kwa nia ya kuboresha maeneo ya kujifunzia na kufundishia kwa shule zetu za sekondari. Aidha fedha hizi zitawezesha kupunguza changamoto ya upungufu wa madarasa 206 katika halmashauri yetu kwa sasa **(Kiambatisho 1) OR – TAMISEMI.**

2. <u>**Hali halisi ya maeneo ya ujenzi kwa shule zetu**</u>.

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kupitia kamati yake ya ujenzi iliyoundwa na Mh: Mkuu wa Wilaya ilifanya ya ziara ya siku **02** kuanzia tarehe **19.10.2021** hadi **20.10.2021** kwa madhumuni ya kukagua Meneo yatakapojengwa Madarasa **146** kwa fedha za Uviko-19 zilizoletwa na Mh.Rais .Katika ziara hiyo shule zilizotembelewa ni **33** kati ya hizo shule **04** ni mpya zinazotarajiwa kupokea wanafunzi kidato cha kwanza **2022** na shule **29** ni za zamani.

Aidha ilielezwa kuwa katika ziara hiyo Kamati imetembelea shule **33**, kati ya hizo shule **25** ni maeneo yake ya ujenzi yapo vizuri na shule **08** zimekuwa na changamoto kama ifuatavyo:-

**JEDWALI : KUONYESHA CHANGAMOTO ZA UJENZI KWENYE SHULE NANE**

| Na. | SHULE | CHANGAMOTO | UTATUZI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mbezi juu | -Eneo lina mabonde makubwa<br>-Mipaka sahihi ya shule haijulikani | **-Lipelekwe katapila kwa ajili ya kusawazisha eneo**<br>**-Mpima aende kufufua mipaka** |
| 2 | Makongo Juu | -Eneo lina mabonde makubwa | **-Lipelekwe katapila kwa ajili ya kusawazisha eneo** |
| 3 | Songoro Mnyonge | - Eneo lina mabonde makubwa<br>- Mipaka sahihi ya shule haijulikani | **- Lipelekwe katapila kwa ajili ya kusawazisha eneo**<br>**- Mpima aende kufufua maeneo** |
| 4 | Makumbusho | -Eneo lina mabonde makubwa<br>- Mipaka sahihi ya shule haijulikani | **- Lipelekwe katapila kwa ajili ya kusawazisha eneo** |
| 5 | Kijitonyama | - Mipaka sahihi ya barabara karibu na shule haijulikani | **-Mpima aende kutambua maeneo** |
| 6 | Kigogo | -Shule haina eneo la ujenzi | **-Linunuliwe eneo kwa wakazi wa jirani (*Compensation*)** |
| 7 | Hananasif | -Shule haina eneo la ujenzi | **- Linunuliwe eneo kwa wakazi wa jirani (*Compensation*)** |
| 8 | Mzimuni | -Shule haina eneo la ujenzi | **- Ufanyike Ujenzi wa Ghorofa** |

3. **Mapendekezo ya Kamati.**

Ilielezwa kuwa kutokana na ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa madarasa 146 kwa shule zetu za sekondari kamati imekuja na mapendekezo yafuatayo,

Fedha za shule **10** zenye kiasi cha Tshs **1,000,000,000/=** ambazo zimekuwa sawa na mapendekezo ya kamati inashauri ujenzi wake uendelee ambazo ni:-

**JEDWALI: KUONYESHA SHULE ZENYE TAARIFA SAWA KATI YA TAMISEMI NA KAMATI**

| S/NO | SHULE | IDADI YA MADARASA | KIASI CHA FEDHA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kisauke | 02 | 40,000,000.00 |
| 2 | Kambangwa | 06 | 120,000,000.00 |
| 3 | Kawe Ukwamani | 06 | 120,000,000.00 |
| 4 | Kondo | 06 | 120,000,000.00 |
| 5 | Bunju A | 06 | 120,000,000.00 |
| 6 | Mbezi juu | 06 | 120,000,000.00 |
| 7 | Makongo Juu | 06 | 120,000,000.00 |
| 8 | Mbweni teta | 05 | 100,000,000.00 |
| 9 | Mikocheni | 04 | 80,000,000.00 |
| 10 | Twiga | 03 | 60,000,000.00 |
| | **JUMLA KUU** | **50** | **1,000,000,000.00** |

1. Madarasa **22** yaelekezwe kwenye shule mpya **03** ambazo ni **Songoro Mnyonge -8, Daniel Chongoro - 8 na Michael Tarimo - 6.**
2. Madarasa **74** yaliyobaki yameongezwa kwenye shule zenye maeneo ya kujenga katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni zikiwa na shule mpya tazama kiambatisho **No. 2.**
3. Mapendekezo ya mabadiliko hayo yawasilishwe **OR-TAMISEMI** kwa ajili ya kupata kibali cha kuhamisha fedha hizo ziende kwenye maeneo yaliyokusudiwa na kamati.

**Maoni ya Wajumbe.**

- Ilifafanuliwa kuwa kwa Kata za Kinondoni na Tandale zimetengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Shule mpya.
- Kata ya Magomeni. Madarasa yawe sita yaani lijengwe jengo moja la ghorofa ambalo litakuwa na madarasa yote hayo sita.
- TAMISEMI waombwe kwamba Manispaa ya Kinondoni inaomba mpango wa kujenga shule za ghorofa.

**Azimio.**

Wajumbe waliridhia kutoa idhini ya Mabadiliko ya Ujenzi wa Vyumba vya Madarasa kwa fedha za Uviko – 19 kama ilivyowasilishwa. Tazama Kiambatanisho.

(c) **Taarifa ya Nyongeza ya Mpango wa Manunuzi kwa mwaka 2021/2022**

Iliwasilishwa Taarifa ya Nyongeza Mpango wa Manunuzi kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi katika Sekta ya Elimu,Afya na Upangaji wa machinga. Itakumbukwa kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluhu Hassan ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa madarasa katika shule za Sekondari , chumba cha dharura (*Emergency Unit*) cha wagonjwa na ujenzi wa vibanda vya machinga kama sehemu ya mapambano dhidi ya Uviko -19. Taarifa hii inaletwa ili kutimiza matakwa ya sheria ya manunuzi ya mwaka 2013 kifungu Na.60(4) kwa kuzingatia hilo naleta kwenu taarifa ya nyongeza ya mpango wa manunuzi kwa mwaka 2021/2022.

**Nyongeza ya Mpango wa Manunuzi.**

Nyongeza ya mpango wa manunuzi umeandaliwa kwa kuzingatia ongezeko la miradi ambayo haikuwepo kwenye mpango wa manunuzi ulioandaliwa wa mwaka 2021/202 ambao uliwasilishwa kwenye bodi ya zabuni kupitia hati ya maazimio ya tarehe 15 julai 2021 ikiwa ni kutekeleza matakwa ya sheria na. 7 ya 2011 kifungu na. 49(1-30), kanuni za manunuzi ya umma ya mwaka 2013, marekebisho yake ya mwaka 2016 na kanuni za uanzishwaji wa bodi za zabuni za Serikali za Mitaa za mwaka 2007. Halmashauri ya Manispaa imepokea

fedha kiasi cha tsh3,220,00,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 146 na jengo la afya la dharura kama ilivyotolewa na ofisi ya Tamisemi Dodoma. Fedha hizi zimepokelewa nje ya mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2021/2022 hivyo zitapelekea mamadiliko katika mpango wa manunuzi kwa kuongezeka kwa kiasi cha cha **Tsh.3220,000,000.00** kwa shughuli za ujenzi. Mpango wa manunuzi wa awali ulikuwa na kisai cha **Tshs 23,757,620,520.27.** nyongeza ya fedha hizo zitapelekea mpango wa manunuzi wa manispaa ya kinondoni kuwa na jumla ya **Tshs. 26,977,620,520.00.**

Mpango umepitishwa na bodi ya zabuni kupitia hati ya maazimio ya tarehe 15 julai 2021. Hivyo nawasilisha kwako kiasi cha **Tsh.3220,000,000.00** ili kupata idhini ya kufanya marekebisho kwenye mpango wa manunuzi.

Kamati inaombwa ijadili na kuidjinisha mabadiliko ya Mpango wa Manunuzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kama ilivyoelezwa hapo juu ambayo yamejadiliwa na kutolewa maamuzi na Bodi ya Zabuni.maombi yanawasilishwa kwako.

**Azimio.**

Wajumbe walipitisha Taarifa ya Nyongeza ya Mpango wa Manunuzi kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi katika Sekta ya Elimu,Afya na Upangaji wa Machinga. Tazama Kiambatanisho.

**5/PM/21** **Kufunga Kikao.**

Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe wote waliohudhuria kwenye Kikao hiki, alieleza kuwa Manispaa sasa tuangalie uwezekano wa kujenga vyoo kwa ajili ya shule. Baada ya kusema hayo alifunga Kikao saa 7.18 mchana.

**UMETHIBITISHWA**

**KATIBU** **MWENYEKITI**

**TAREHE** 25/10/2021